**POTENT ACADEMY REVISION SERIES**
**SHUGHULI ZA KISWAHILI**
**GRADE 9 | MODEL 06**

**Jina_________________________________________________ Tarehe ____________________**

*Jibu maswali yote kwa nafasi uliyopewa:*

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 hadi 7. Kwa kila nafasi, chagua jibu sahihi kati ya uliyopewa.**

Kitongoji cha Randaranda ______ 1 ______ kizaazaa cha mwaka ______ 2 ______ ambapo bwana mmoja ______ 3 ______ Kizito, alijitia ______ 4 ______ na kukata kamba papo hapo. Hili lilitokana na ugomvi ______ 5 ______ baina yake na mkewe. Iliripotiwa kuwa, ______ 6 ______ kujimaliza, aliwakatakata watoto wake ______ 7 ______ jisu na kumdunga mkewe kifuani kisha akajitendea tendo hilo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. waliona | B. kilitazama | C. kilishuhudia | D. waliangalia |
| 2. | A. pale | B. hapa | C. huko | D. mle |
| 3. | A. : | B. ? | C. . | D. , |
| 4. | A. mbioni | B. kitanzi | C. hamnazo | D. shimoni |
| 5. | A. uliojiri | B. iliyotokea | C. uliyozuka | D. iliotokea |
| 6. | A. kabla ya | B. mbele ya | C. baada ya | D. nyuma ya |
| 7. | A. na | B. kwenye | C. katika | D. kwa. |

**Kutoka swali la 8 hadi 17, jibu maswali kulingana na maagizo,**

8. Tumia viulizi sahihi kukamilishia sentensi hii.
   a. Chakula hiki kimepikiwa ___________________________ ?
   b. Sherehe ya Madaraka itaadhimishwa ____________________________?
9. Tambua alama zifuatazo za uakifishi.
   a.: ___________________________________________________
   b.; ___________________________________________________
10. Tumia vivumishi vilivyo mabanoni kukamilishia sentensi.
    a. Tumetembelewa na wageni ____________________ (nane) kutoka Ughaibuni.
    b. Pua __________________ (angu) ina kidonda kidogo.

*Download more Revision papers from www.potentacademy.com/resources*
Join our WhatsApp Revision group | Contact 07 01 23 83 83

11. Jaza nafasi kwa kutumia viambishi sahihi vya ngeli.

    a. Mihadarati ____________ mepigwa marufuku nchini humo.

    b. Uyoga niliochuma ____________ meoza.

12. Andika vinyume vya maneno yaliyopigiwa mistari.

    a. Asanati anaendesha baiskeli yake <u>kwa kasi</u>.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

    b. Wanafunzi <u>walifurahi</u> baada ya kupewa tuzo.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

13. Jaza vihasho kwa kauli za kutendeka za vitenzi vilivyo mabanoni.

    a. Darasa lili ____________________ (fagia) kwa urahisi

    b. Chakula kime ______________________ (pika) haraka.

14. Kanusha kauli zifuatazo kwa usahihi.

    a. Wewe umekuwa mwanafunzi mwema.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

    b. Ukipanda pantosha utavuna pankwisha.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

15. Andika kanuni mbili zinazozingatiwa katika kubadili usemi halisi kuwa usemi wa taarifa.

    a. ______________________________________________________________

    ______________________________________________________________

    b. ______________________________________________________________

    ______________________________________________________________

16. Andika matumizi mawili ya ritifaa.

    a. ______________________________________________________________

    ______________________________________________________________

    b. ______________________________________________________________

    ______________________________________________________________

*Download more Revision papers from [www.potentacademy.com/resources](www.potentacademy.com/resources)*
Join our WhatsApp Revision group | Contact 07 01 23 83 83

17. Tambua aina za maneno zilizopigiwa mistari.

    a. Huyu hapa ni ng'ombe wangu, <u>yule</u> ni wa mjomba wangu.

___

    b. Mgonjwa alitembea <u>kivivu</u> ila alifika hospitalini.

___

**<u>Kutoka swali la 18 hadi la 20 chagua jibu sahihi.</u>**

18. Ni sentensi ipi iliyo katika hali ya ukubwa?

    A. Jokofu hilo liliuzwa sokoni jana.

    B. Jino lililokuwa likiuma lilitibiwa.

    C. Joto hilo lilikuwa kali sana.

    D. Jipira limepigwa kwa ustadi mkuu.

**19.** Chagua usemi halisi wa: **Kefa alimwahidi Juma kwamba angemsaidia kukuza kipawa chake cha uchoraji.**

    A. "Atanisaidia kukuza kipawa chako cha uchoraji," Kefa alimwahidi Juma.
    B. "Nitakusaidia kukuza kipawa chako cha uchoraji," Kefa alimwahidi Juma.
    C. "Atakusaidia kukuza kipawa chako cha uchoraji, " Kefa alimwahidi Juma.
    D. "Nitamsaidia kukuza kipawa chako cha uchoraji," Kefa alimwahidi Juma.

20. Neno, **huruma** katika sentensi, **Matu alimwonea huruma**, ni nomino dhahania.

    *Chagua jibu linaloonyesha aina za nomino zilizopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo:*

    <u>Baraza</u> la wazee liliamua <u>kesi</u> hiyo kwa wakati ufaao.

    A. pekee, wingi
    B. kawaida, pekee
    C. wingi, makundi
    D. makundi, kawaida

*Download more Revision papers from www.potentacademy.com/resources*
Join our WhatsApp Revision group | Contact 07 01 23 83 83